

MATUMAINI PROG NO:2529

TITLE: WHO IS ON THE LORD'S SIDE?

SUMMARY: KINAZUNGUMZIA KUHUSU YULE AMBAYE NI MCHA MUNGU KAMILI.

TEXT: KUTOKA 32:11-29

MADA: NI NANI ALIYE KATIKA UPANDE WA BWANA?

.....

Natushukuru kwanza kabla ya kulianza somo la leo.

OMBI....Mungu Mkuu na tena Mshahuri wa ajabu Muumbaji wetu,,,tunasema ni asante kwa ajili ya nafasi hii ambayo umetupatia ili kutufunulia kuhusiana na Mapenzi yako kwetu kama wanao,,, fungua mioyo yetu ili tukaweze kukuelewa vyema.

Ni kwa Yesu tumeomba, Amina.

Ni kwa upendo ulioje kwa ajili ya Mungu wetu kutupatia nafasi nyingine ili kujifunza kutoka Nenoni mwake. Ninayo imani ya kwamba,, unaendelea vyema. Karibu sana kwenye somo hili la leo ambalo tunaulizana swali ya kwamba,,,,*Je!,,ni nani aliye katika upande wa Bwana?*

Kipindi hiki ni cha Matumaini kutoka TWR Kenya.

Somo linatoka kwenye Kutoka 32:11-29.

Nikiwa nakaribia tu pale mwisho,,,nitakuwa na kupatia anwani yangu ya mawasiliano kati yangu nawe.

Nataka kwanza kabisa ukabarikiwe kwa njia kama hii... ..

WIMBO:

Ni watumishi Papi Clever & dorcas ft Merci pianist na wimbo sitasumbuka

Asante sana watumishi kwa wimbo huo mtamu.....

Mimi naitwa, Vincent Amara.

Msikilizaji wangu,,,maisha kwa mara nyingi huwa kama njia panda inayotutenganisha yaani T-junction kwa lugha ya wale wanaokielewa kiingereza.

Mawazo yetu wenyewe hufika kikokomo,, na,, tunakosa hata kujua,, ni uamuzi upi ambao tunaweza kuuchukua ili kuelekea katika njia ambayo ni sahihi au niseme njia iliyo sawa.

Katika nyakati kama hizo, ni jambo la msingi sana kuwapata viongozi sahihi wa kutuongoza.

Maisha yetu si kama meza ya vyakula mbalimbali ambapo kila mtu anaweza kuchagua kile kinachomvutia kwa wakati huo. Leo tunashuhudia mabadiliko makubwa sana ya kitamaduni na pia ya kiroho humu ulimwenguni. Hata wanasayansi, wanafalsafa na wanatheolojia,,kupitia kwa masomo yao,,wanajaribu kutuletea mitazamo mipya inayovutia akili zetu,,,lakini ndugu yangu,,,elimu hiyo ni ya kuupotosha tu ukweli.

Mwandishi mmoja wa mambo ya kidini, kwa jina Russell Chandler, katika kitabu chake "Understanding the New Age", anatusaidia sana katika kuiona hatari hii.

Anasema kuwa mambo ya kiroho yanatafsiriwa upya mbele ya macho yetu,,, ulimwengu unahamishwa kutoka kwenye misingi ya Kikristo na kwenda kwenye misingi ya kipagani au kwa lugha rahisi misingi ya kikafiri,, ambapo hakuna misingi ya ukweli iliyo thabiti au kwa kiingereza,,,No absolutes.

Dadangu,,,kila mmoja wetu ambaye anaonekana kuwa sawa,,,,iwe anaomba kwa kwa ukweli,iwe ni kwa miungu ya kiasili, au kwa njia ya Utatu Mtakatifu,, mradi tu "inamfaa" basi haina shida! Lakini historia inathibitisha wazi kwamba maadili yanayobadilika kulingana na mazingira yaani "Relative morality,, huleta machafuko na mwishowe,,,jamii hupata kuanguka.

Ni katika muktadha wa mabadiliko haya ambapo tunapaswa kuisikia sauti ya Musa akisimama mbele ya taifa la Israeli pale Mlimani Sinai, baada ya watu kuziacha amri za Mungu na kujitengenezea sanamu ya ndama wa dhahabu ili waiabudu.

Katika kitabu cha Kutoka 32:11-29, Musa anasimama na kuliuza swali hili zito kwamba,,, "Ni nani aliye katika upande wa BWANA?"

Nataka tukaweze kuzingatia aya za kimsingi pekee,,,nami nakushirikisha kuanzia aya ya 25-29.

Aya hizi zinasomeke hivi;

25 Basi Musa alipoona ya kuwa watu hawa wameasi, maana Haruni amewaacha waasi, ili wawe dhihaka kati ya adui zao,

26 ndipo Musa akasimama katika mlango wa marago, akasema, Mtu awaye yote aliye upande wa Bwana, na aje kwangu. Wana wa Lawi wote wakamkusanyikia

27 Akawaambia, Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi, Kila mtu na ajifunge upanga wake pajani mwake, akapite huko na huko toka mlango hata mlango kati ya marago, mkamchinje kila mtu ndugu yake, na kila mtu mwenziwe na kila mtu jirani yake.

28 Na hao wana wa Lawi wakafanya kama vile alivyosema Musa, wakaanguka siku ile kama watu elfu tatu.

29 Musa akasema, Jiwekeni wakfu kwa Bwana leo, naam, kila mtu juu ya mwanawe na juu ya ndugu yake; ili awape baraka leo.

Rafiki yangu,kutokana na fungu hili la neno,,,tunapata kuona ya kwamba,Musa alipokuwa mlimani akizipokea sheria za Mungu,Wana-Waisraeli walimshawishi Haruni awatengenezee ndama wa dhahabu ili wamwabudu.

Neno la Mungu linatuambia,,,Mungu alikasirika na kutaka kuwaangamiza, lakini Musa akawaombea,,, na Mungu akawaonyesha rehema Yake.

Musa aliposhuka kutoka mlimani na kuiona ibada ya sanamu ikiendelea, Bibilia inatuambia,,,alikasirika, akazivunja zile mbao za sheria, na hata zaidi akaiharibu ile ndama ya dhahabu waliojitngengenezea, kisha akamkemea Haruni kwa kuwaongoza watu katika dhambi.

Dadangu,,,kupitia kwa swali hili kwamba"Ni nani aliye katika upande wa BWANA?", Musa alionyesha sifa tatu kubwa za kitabia ambazo tunapaswa kuziiga hat awa leo ili tuweze kusimama upande wa Mungu kikamilifu.

Kipengele cha kwanza kabisa ambacho tunajionea,,ni kuhusiana na vile ambavyo,,, Musa alikuwa akishirikiana kwaukaribu sana naye Mwenyezi Mungu.yaani kwa kiingereza,,,an Intimate Communion.

Musa alikuwa na mwaliko maalum kutoka kwa Mungu,,wa kupanda mlimani ili kufanya urafiki na zaidi sana ushirika naye. Neno linatuambia ya kwamba,,,alikaa huko mlimani, ndani ya wingu la utukufu wa Bwana, kwa muda wa siku arobaini

usiku na mchana. Ndugu pamoja na dadangu,,,bila shaka huu ulikuwa ni ushirika wa karibu sana wa ana kwa ana.

Bibilia yetu inatuambia ya kuwa,,,, wakati Musa akiwa mlimani, watu kule chini waliigeukia ibada ya sanamu. Mungu alipoona uasi wao, ghadhabu yake iliwaka na akataka kuwaangamiza wote na kumfanya Musa kuwa taifa kubwa badala yao. Lakini hapo ndipo tunapouona moyo wa Musa. Badala ya kujitafutia umaarufu,,,alisimama kama mwombezi ama niseme,,, "Intercessor'kwa ajili ya Israeli.

Ndugu yangu,,,,mtumishi wa Mungu Musa alimsihi Mungu akiwakumbusha ahadi Alizowapa Ibrahimu, Isaka, na Israeli, na jinsi Wamisri watakavyomdhihaki Muumbaji wao ikiwa atawaangamiza watu wake jangwani.

Maombi haya ya karibu yaliwazuia kutokana na hukumu yake Mwenyezi Mungu.Ushirikiano huu ulimfanya Musa aelewe utakatifu wa Mungu kwa kiwango cha juu sana.

Msikilizaji mpendwa,,, leo tunahitaji watu wanaoshirikiana na Mungu kwa siri ili waweze kutenda kwa ujasiri kwa niaba yake na kuzidisha zaidi,,,,,kwa uwazi bila kuficha chochote.

Kipengele cha pili ndugu yangu,,, tunamwona,,, Musa Akikabili Uovu kwa Ghadhabu ya Haki (Indignant Confrontation). Musa aliposhuka mlimani na kuona yule ndama wa dhahabu na watu wakicheza ngoma, hasira yake iliwaka sana ndani ya roho yake.

Alizitupa zile mbao mbili za sheria zilizoandikwa kwa kidole cha Mungu, akazivunja chini ya mlima,, ishara ya kwamba watu walikuwa tayari wamezivunja amri hizo mioyoni mwao.

Neno linatuambia kuwa,,siku chache zilizopita, watu walikuwa wamesikia amri kuu mbili za kwanza: "Usiwe na miungu mingine ila mimi" na "Usijifanyie sanamu ya kuchonga", na wote walikuwa wamejibu, "Yote aliyoyasema Bwana tutafanya." Lakini walishindwa vibaya sana kusubiri.

Musa hakunyamazia uovu; alichukua yule ndama wa dhahabu, akamteketeza kwa moto, akamsaga hadi akawa unga laini, akautawanya juu ya maji, na kuwalazimisha Waisraeli wanywe maji hayo!

Kisha, alimkemea vikali kaka yake Haruni kwa kuendelekeza uovu huo kwa sababu ya shinikizo la watu. Haruni alionyesha udhaifu mkubwa wa uongozi kwa kutoa udhuru usio na msingi, akionekana kama kiongozi legelege aliyeruhusu maelewano na dhambi.

Musa alisimama kidete na kukabili uovu uliokuwa katikati ya kambi.

Kipengele cha tatu na cha mwisho kwa leo,,, tunamshuhudia,,, Musa Akiamuru Utakaso wa Haraka. Musa alisimama katika lango la kambi na kupaza sauti yake iliyovuma kambi nzima: "Ni nani aliye upande wa BWANA? Na aje kwangu!" Kwa kusema hivyo, yeye mwenyewe alikuwa tayari amesimama upande wa Bwana. Wana wa Lawi, ambao walikuwa ndugu zake, walijitenga na umati na kukusanyika kwake.

Musa aliwapa maagizo makali na thabiti: Aliwaambia hivi,, "Fungeni kila mtu upanga wake mapajani... mkawaue kila mtu ndugu yake, na kila mtu rafiki yake, na kila mtu jirani yake." Unaweza kuona jambo hili kuwa la kikatili sana, lakini ni lazima uelewe uzito wa dhambi hiyo.

Mpendwa,, tendo la kuabudu sanamu ni la kuchafua kiroho,,, tena pakubwa zaidi taifa zima. Wana wa Lawi walitii, na watu wapatao elfu tatu walianguka siku hiyo. Jambo hili linatufundisha jinsi uasi ulivyo mbaya mbele za Mungu tunapogeuka baada ya kujua ukweli.

Baada ya utakaso huo mkali, Musa aliwaita watu kwa upendo kuelekea kwenye upatanisho akisema: "Jiwekeni wakfu leo kwa Bwana... upate kuwabariki leo." Mungu wetu ana rehema nyingi sana; anataka tujinyenyekeze, tujitakase, na kuyaweka maisha yetu kwake upya.

Rafiki yangu,,,, Musa anatuuliza sote leo swali lile lile: kwamba "Ni nani aliye katika upande wa Bwana au Yuko upande wa Bwana ni nani?" Musa alikuwa na haki ya kuuliza hivi kwa sababu yeye mwenyewe alishirikiana na Mungu kwa karibu, alikabili uovu bila uoga, na aliamuru utakaso katika kambi.

Leo tunahitaji wanaume na wanawake wa namna hii katika kambi yetu ya Kikristo. Je, wewe uko upande gani? Kumbuka kuwa ukiwa upande wa Mungu, hata kama uko peke yako, wewe ndiye uliye na wengi kuliko umati wote unaokuzunguka.

Ningependa kumaliza kwa ku-kuhimiza na neno kutoka kwenye 1 Petro 2:9. Neno hili linasema hivi; "Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu."

Amina!

Ombi.....

Mungu wetu Uliye Mkuu kushinda vyote,,,,tunakushukuru sana kwa sababu ya fundisho hili la leo,,,ambalo limetufundisha ya kwamba ni wewe tu wakuabudiwa. Tusaidie katika kulizingatia na zaidi sana Kutenda hivyo. Asante kwa sababu ya kutuonyesha mweelekeo huu wa kuupatana nao uso wako.

Ni kupitia kwa jina lake tumeomba.....Amen.....

Rafiki yangu,,hiki Kimekuwa ni kipindi chako cha kujifunza neno Lake Mwenyezi Mungu. Kipindi cha matumaini kutoka Twr. Leo mada yetu imekuwa ni kuwa,,,Ni nani aliye katika upande wa Bwana.?

Tumeutoa kwenye Kutoka 32:11-29.

Tafadhali wasiliana nami kupitia kwa anwani nitakayo kusomea mwishoni mwa kipindiki hiki cha leo. Sababu ya kukupatia anwani hiyo,,ni kwa ajili ya kusaidiana nawe.

Kabla yake,,ni wimbo nikujue zaidi....

WIMBO.....

Ni mtumishi Ali Mkhwana,,Mungu Akubariki sana. Ni wimbo nikujue zaidi....

ANDIKA BARUA AU UJUMBE WAKO UKIANZA NA NENO MATUMAINI TWR NA

KUTUMA KWA:

SLP 21514 CODE 00505

NAIROBI KENYA x2

Simu/Sms 0721970520 x2
Barua Pepe-barua@twr.co.ke
Kwenye Youtube ni @twr.ke

Mungu na akubarki sana Msikilizaji popote ulipo na,, hadi wakati mwingine, jina langu ni Vincent Amara.....Kwaheri